NISHATI
HABARI ZA NISHATI

News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 25 | Aprili 1 - 30, 2021

# DKT. KALEMANI AZINDUA RASMI KITAIFA, REA III

## MZUNGUKO WA PILI



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wanakijiji wa Ugaka wilayani Igunga mkoani Tabora (hawapo pichani) wakati wa ziara ya uzinduzi rasmi wa kitaifa, wa mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliofanyika, Machi 15, 2021.*







LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**

# Dkt. Kalemani azindua rasmi kitaifa, REA III mzunguko wa Pili

**Na Zuena Msuya, Tabora**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amezindua rasmi kitaifa usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili utakaokamilisha usambazaji wa umeme katika Vijiji vyote 1,974



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa kitaifa, mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliofanyika, Machi 15, 2021 katika kijiji cha Ugaka wilayani Igunga mkoani Tabora.*




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ( kushoto) akibadilishana mawazo na Mbunge wa Manonga, Saif Gulamali ( kulia) wakati wa ziara ya uzinduzi rasmi wa kitaifa, wa mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliofanyika, Machi 15, 2021 katika kijiji cha Ugaka wilayani Igunga mkoani Tabora.*






BODI YA UHARIRI

**Makamu Mwenyekiti**
**Mhandisi Leonard Masanja**
Kaimu Katibu Mkuu

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# Safari ya umeme kuwaka nchi nzima yaendelea

Ili kuhakikisha kuwa, wananchi wote wanapata huduma ya umeme ya uhakika, Serikali inaendelea kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme mijini na vijijini.

Hivi karibuni, Waziri wa Nishati, Mhe. DKt. Medard Kalemani alizindua mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambao umelenga kusambaza umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijasambaziwa umeme nchini.

Mradi huo wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili unasambaza umeme kwenye vijiji 1,974 ambavyo bado havijasambaziwa umeme kati ya vijiji 12,268 vilivyopo nchini.

Akizindua mradi huo, wilayani Igunga, Mkoa wa Tabora, Waziri Kalemani alisema kuwa ndani ya miezi 18 ijayo, Serikali itahakikisha kuwa umeme unavifikia vijiji hivyo 1,974 vilivyosalia.

Ili kuhakikisha kuwa, lengo hilo la kuwasambazia umeme wananchi wa vijiji husika ndani ya miezi 18 linafanikiwa, Dkt, Kalemani amewaagiza wakandarasi kuheshimu muda uliowekwa na Serikali wa kufanya kazi husika.

Alionya kuwa, mkandarasi atakayekiuka msimamo huo atakuwa amekiuka mkataba na atachukuliwa hatua, ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa kazi hiyo ya ukandarasi.

Ili kuhakikisha, kazi ya usambazaji umeme katika vijiji vilivyosalia inafanyika kwa ufanisi mkubwa, hivi sasa kila wilaya itakuwa na mkandarasi wake tofauti na hapo awali.

Aidha, Wakandarasi hao pia watatakiwa kujitambulisha kwa uongozi wa Vijiji, Wilaya na Mikoa wanayofanyia kazi, ili viongozi hao waweze kupata fursa ya kufuatilia utekelezaji wa mradi huo.

Ni nia ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kuwa, nchi yote inafikiwa na huduma ya umeme, hatua ambayo itazidi kuinua si tu uchumi wa nchi, lakini pia kupambana na uharibifu wa mazingira utokanao na kukata miti kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

Shime wananchi, tuunge mkono juhudi hizi za Serikali kwa kuhakikisha kuwa tunaunganisha umeme kwa ajili ya matumizi ya kijamii na kiuchumi, tuhakikishe kuwa tunatandaza nyaya majumbani ili miundombinu ya umeme inapofika kwenye maeneo yetu, kazi inayobaki ni kuunganisha tu umeme.

# Dkt. Kalemani azindua rasmi kitaifa, REA III mzunguko wa Pili

vilivyosalia nchini.

Uzinduzi huo wa Kitaifa ulifanyika katika Kijiji cha Ugaka, wilayani Igunga Mkoani Tabora, Machi 15, 2021.

Dkt. Kalemani alisema kuwa mradi huo utagharimu shilingi Trilioni 1.24 za kitanzania na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia sasa katika mikoa yote nchini.

Pamoja na mambo mengine, Dkt. Kalemani alisema kuwa kila wilaya itakuwa inapewa mkandarasi wake kutekeleza mradi huo ili kukamilisha kazi hiyo kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa katika miradi iliyotangulia ambapo mkandarasi alikuwa akipewa zaidi ya mkoa mmoja kufanya kazi hiyo jambo ambalo lilichangia kusuasua na kutokamilika kwa wakati kwa mradi.

Alisema kuwa kwamantiki hiyo, hakuna kuongeza muda wa ziada kwa mkandarasi yeyote atayeshindwa ama kuchelewa kukamilisha mradi huo kwa muda uliopangwa,na atayeshindwa



*Baadhi ya wanafunzi wa shule ya msingi katika Kijiji cha Ugaka wakiwa wamenyoosha juu jarida linalochapisha habari za Wakala wa Nishati Vijijini( REA) kufurahia uzinduzi rasmi wa kitaifa wa mradi wa usambazaji umeme vijijini , Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliofanyika, Machi 15, 2021, katika kijiji hicho wilayani Igunga mkoani Tabora.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akiweka jiwe la msingi kuashiria uzinduzi rasmi wa kitaifa, mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliofanyika, Machi 15, 2021 katika kijiji cha Ugaka wilayani Igunga mkoani Tabora.*

kukamilisha mradi huo kama mkataba unavyoelekeza atafutiwa mkataba wake na kufikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

"Kwa sasa hakuna kuongeza muda kwa mkandarasi yeyote atayechelewesha mradi, tutachukua hatua za kisheria kwa mujibu wa mkataba, ikiwemo kufuta mkataba wa mkandarasi na kumfikisha mahakamani, tumeamua kutoa mkandarasi mmoja kwa kila wilaya hii yote ni kuhakikisha kazi hii inakamilika kwa wakati ndani ya miezi 18, tutakuwa tumemaliza kusambaza umeme katika vijiji vyote 1,974 vilivyosalia nchi nzima". Alisema Dkt. Kalemani

Aliendelea kuwasisitiza wananchi kulipia gharama ya shilingi 27,000 tu katika vijiji na mitaa, na kamwe wasikubali kurubuniwa maafisa wasio waaminifu pamoja na vishoka watakaotaka kuwatoza gharama kubwa zaidi.

Pia wananchi hao waendelee kutandaza nyaya katika nyumba zao ili kujiweka tayari kuunganishiwa umeme.

Aidha aliwataka wakandarasi hao kujitambulisha kwa uongozi wa vijiji, wilaya na mkoa kabla ya kuanza kazi na kuwaeleza viongozi hao ratiba za

# Dkt. Kalemani azindua rasmi kitaifa, REA III mzunguko wa Pili



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akikabidhi cheti kwa Mhandisi Alistidia Kashemeza akiwa ni miongoni mwa Meneja wa Kanda, Mkoa na Wilaya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), waliofanya kazi vizuri ya kusimamia mradi wa usambazaji wa umeme vijiji katika mradi uliotangulia, wa nne kula ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na wa pili kulia ni Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja.*

kazi zao kwa eneo husika ili kuwa rahisi viongozi hao kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huo.

Alisitiza kuwa wakandarasi hao wahakishe kuwa kazi zote zisizohitaji taaluma maalum zipewe kwa wakazi wa eneo husika na walio karibu na eneo hilo ili kunufaika na uwepo wa mradi huo.

Katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa umeme muda wote katika wilaya ya Igunga, Dkt. Kalemani aliahidi kujenga kituo kidogo cha kupoza umeme katika wilaya hiyo ili kupunguza tatizo la umeme kutokuwa na nguvu linalosababishwa na umeme huo kutoka umbali mrefu.


Katika hatua nyingine, Dkt. Kalemani alifanya mkutano na wanakijiji wa kijiji cha Isanzu, wilayani Nzega mkoani humo na kuwaeleza kuwa mkandarasi wa kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika wilaya hiyo amekwishapatikana na muda wowote ataanza kufanya kazi kwakuwa fedha ya kutekeleza mradi huo ipo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Philemon Sengati aliwataka wananchi wa mkoa huo hasa katika vijiji ambavyo havijafikiwa na mradi huo kuchangamkia fursa ya kuweka umeme katika nyumba zao na kwamba Serikali imetenga fedha nyingi kuhakikisha umeme unawafika katika kila kijiji.

Sengati aliwaeleza kuwa lengo la serikali ni kufikisha umeme kwa kila mtanzania ili atumie Umeme huo katika kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo na pia kutunza mazingira kwa kuwa umeme ukitumika kama nishati ya kupikia, utasaidia kuhifadhi mazingira kwa kutunza misitu nchini kwa kuepusha ukataji wa kuni na kuchoma mkaa.

Mkuu wa mkoa huo, amewataka wawekezaji kwenda kuwekeza katika mkoa wa Tabora kwa kuwa una fursa nyingi za uwekezaji kutokana na shughuli mbalimbali za Kilimo,ufugaji pamoja na uchimbani madini kwa kuwa kuna umeme wa kutosha.

Na katika uzinduzi huo, Dkt. Kalemani alitumia fursa hiyo kukabidhi vyeti vya kutambua kazi nzuri ya Mameneja na Wakuu wa Kanda, Mkoa na Wilaya wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Wakala wa Nishati Vijijini (REA),waliofanya kazi vizuri ya kusimamia mradi wa usambazaji wa umeme vijijini na kuunganisha wateja kwa mradi uliotangulia.




*Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipopata maelezo toka kwa Waziri wa Nishati Dkt. Menard kalemani  kabla ya kuzindua mradi wa kuzalisha umeme MW 240 wa Kinyerezi ll eneo la Kinyerezi jijini Dar es salaam,  Aprili 3, 2018*

# Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaridhishwa na kasi ya Ujenzi wa JNHPP

**Na Zuena Msuya Pwani,**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula amesema Kamati hiyo imeridhishwa na kasi ya Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere( JNHPP) na kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa mradi huo.

Kitandula alisema hayo tarehe 12 Machi, 2021 mkoani Pwani, wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati hiyo iliyolenga kukagua maendeleo ya Miradi mbalimbali katika sekta ya Nishati inayotekelezwa kwa kutumia fedha za ndani.

Alisema kuwa baada ya kuona hali halisi ya utekelezaji wa mradi huo kwa sasa Kamati hiyo inatembea kifua mbele ikijivunia kazi kubwa iliyofanyika na inayoendelea kufanyika kukamilisha mradi huo kwa wakati.

"Kwa mara ya kwanza wakati wazo la kutekelezwa kwa mradi



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa JNHPP mkaoni Pwani, Machi 12, 2021.*

# Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaridhishwa na kasi ya Ujenzi wa JNHPP

huu lilivyotolewa, Kamati tulifurahia sana kuona ndoto ya Baba wa Taifa inaenda kutimia na kuweka historia mpya ya nchi yetu, na tuliadidi kuwaeleza watanzania mpaka watuelewe juu ya mradi huo mkubwa unaogharimu fedha nyingi, kwakuwa sisi ndiyo wenye dhamana ya kupitisha bajeti ya Serikali pamoja na miradi yake, baada ya kuona kinachoendelea hapa sasa hivi, tunatembea kifua mbele na kuwaeleza watanzania kuwa wajivunie kuwa na mradi huu mkubwa utakaokamilika ndani ya muda uliopangwa na utakuwa na manufaa makubwa sana ndani na nje ya nchi". Alisema Kitandula.

Aidha alisema kuwa, wamefurahishwa na kitendo cha Serikali kulipa kwa wakati fedha za mkandarasi anayetekeleza mradi huo kwa kila hatua ya ujenzi wa mradi inapofikia.

Sambamba na hilo aliipongeza Serikali ya awamu ya Tano, inayoongozwa na Rais, Mhe. Dkt. John Magufuli kwa kuthubutu na kutekeleza mradi huo,



*Mhandisi Mkazi ambaye pia ni mshauri wa mradi huo, Mhandisi John Mgeni akiwaonyesha kitu Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa JNHPP mkoani Pwani, Machi 12, 2021.*

# Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaridhishwa na kasi ya Ujenzi wa JNHPP



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, (katikati) akiwaonyesha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, eneo litakalosimikwa mitambo ya kuzalisha umeme, walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa JNHPP mkoani Pwani, Machi 12, 2021.*

ulioasisiwa na Baba wa Taifa zaidi ya miaka 40 iliyopita, na kuupa kipaumbele kwa kutenga fedha za kutekeleza mradi husika.

Kwa upande wake Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani aliieleza Kamati hiyo kuwa imekuwa ni chachu ya kutekeleza mradi huo baada ya kuridhia na kupitisha bajeti ya kutekeleza mradi huo pamoja na kuwa bega kwa bega na wizara ya Nishati kuhakikisha mradi huo unatekelezwa.

Dkt. Kalemani alisema kuwa mradi wa JNHPP utakaozalisha megawati 2115 umetoa fursa kwa wahandisi wataalam kupata elimu na ujuzi zaidi wa kujenga mradi mwingine kama huo.

Aliweka wazi kuwa takribani Wahandisi wa ndani 200 wamepata mafunzo ya namna ya kujenga miradi kama hiyo katika vyanzo mbalimbali vya Maji yanayopatikana nchini.

Vilevile aliwaeleza wajumbe wa Kamati hiyo kuwa tayari ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme kutoka katika mradi huo hadi katika kituo kikubwa cha kupokea na kupoza umeme kilichopo Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma kupitia Dar es Salaam- Chalinze Pwani umeshaanza kutekelezwa.

"Ninyi Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ndiyo mmefanikisha utekelezaji wa mradi wa JNHPP kwa kuridhia na kupitisha bajeti ya Wizara ya Nishati ambayo ndani yake kulikuwa na fedha nyingi za kutekeleza mradi huu ambazo ni fedha za ndani, bila kuchoka mmekuwa mkifuatilia matumizi ya fedha zinazotumika katika mradi huu ukilinganisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi, tunaamini ushirikiano baina yenu na sisi ndiyo umeleta matokeo chanya kwa watanzania na Taifa kwa jumla". Alisisitiza Dkt. Kalemani.

Katika hatua nyingine aliwaomba wajumbe wa Kamati hiyo kwa kushirikiana na Kamati nyingine, kuwa mabalozi wa kuhamasisha ulinzi wa vyanzo vya Maji ya mito inayotiririsha Maji

# Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaridhishwa na kasi ya Ujenzi wa JNHPP



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (pili kushoto) akitoa maelezo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa JNHPP mkoani Pwani, Machi 12, 2021.*

yake katika mradi wa JNHPP.

Dkt. Kalemani alisema kuwa, kuanzia mwezi Novemba mwaka huu, kingo za maji ya bwawa zitakuwa zimekamilika na kuanza kuvuna maji yatakayotumika kuendesha mitambo ya kufua Umeme pindi mradi huo utakapokamilika Juni 2022, hivyo ni muhimu kutunza vyanzo vya mito na kuwa na matumizi sahihi ya maji ya mito.

Alisema kuwa, zaidi ya futi za ujazo Lita Bilioni 32. 5 za maji kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mito zinahitajika ili kuanza kujaza maji katika bwawa hilo hivyo taasisi, mashirika mbalimbali pamoja na watu wanaoishi kuzunguka vyanzo maji ya mradi huo wanatakiwa kuwa walinzi wakuu, kulinda maji yasipotee bila sababu ya msingi.

Aliongeza kuwa, Mradi huo utakapokamilika mwaka 2022 utazalisha Megawati 2115, na kuifanya Tanzania kuwa na Jumla ya Megawati 4848, huku mahitaji halisi kwa nchi zima yakitarajiwa kuwa ni Megawati 2700.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza gharama ya Umeme na kuongeza usambazaji na matumizi ya Umeme kwa wananchi na utachangia kutunza mazingira kwa kuwa watu wataacha kupikia kuni na mkaa.

# Matengenezo ya mitambo ya umeme nchi nzima yakamilike ndani ya siku Tano - Dkt. Kalemani

**Na Teresia Mhagama, Dar es Salaam**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameagiza kuwa, matengenezo ya mitambo mbalimbali ya kufua umeme nchini yakamilike ndani ya siku Tano ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata umeme wa uhakika.


Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo tarehe 2 Machi, 2021 mkoani Dar es Salaam, mbele ya Bodi na Menejimenti za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Songas, baada ya kukagua kituo cha umeme cha Songas ambacho mitambo yake miwili inafanyiwa matengenezo na hivyo kuzalisha umeme wa kiasi cha megawati 115 badala ya 180.

Akiwa ameambatana na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Waziri Kalemani alisema kuwa, hataki kusikia wananchi wakilalamika kukosa umeme kwa sababu tu ya matengenezo ya mitambo, hivyo matengenezo hayo yakamilike ndani ya siku alizoagiza au kwa siku chache zaidi.

Aidha, kuhusu muda wa kufanya matengenezo ya mitambo ya umeme nchini, Dkt. Kalemani aliiagiza TANESCO na Songas kupishanisha muda wa matengenezo ili kutoathiri hali ya upatikanaji wa umeme nchini.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na moja ya wataalam (kushoto), wanaofanya kazi ya kutengeneza baadhi ya mitambo ya umeme katika Kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na Songas.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akipata maelezo kuhusu matengenezo ya mitambo miwili ya umeme katika kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam. Anayetoa maelezo ni Meneja Mitambo wa Songas, Michael Mngodo.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa Pili kulia) akipata maelezo kuhusu mitambo ya umeme katika kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam. Anayetoa maelezo ni Mkurugenzi Mkuu wa Songas, Anael Samuel (wa kwanza kushoto.Wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi.*

# Matengenezo ya mitambo ya umeme nchi nzima yakamilike ndani ya siku Tano - Dkt. Kalemani

Hata hivyo, Dkt. Kalemani alisisitiza kuhusu utekelezaji wa agizo alilolitoa kwa TPDC la kuhakikisha kuwa vifaa mbalimbali vinavyotumika kwenye miundombinu ya gesi nchini kama vile valvu na mabomba vinatengenezwa nchini ili kurahisisha upatikanaji wa vifaa husika.

Vilevile, alisema kuwa, Wizara ya Nishati haitaacha kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake kwani lengo ni kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinafanya kazi kwa ufanisi na wananchi wanapata huduma wanazostahili.



*Mafundi wakiendelea na kazi ya utengenezaji wa moja ya mtambo wa umeme katika kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam.*

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Songas, Anael Samuel, alimueleza Waziri wa Nishati kuwa, matengenezo ya mitambo miwili ya umeme kwenye kituo hicho, yanaenda sambamba na matengenezo katika bomba la Gesi kutoka Songosongo linalopeleka gesi kwenye mitambo hiyo ya Songas ili kuzalisha umeme.

Alisema kuwa, kutokana na bomba hilo la gesi kutoka Songosongo kufanyiwa matengenezo, kwa sasa megawati 115 zinazozalishwa kwenye kituo hicho zinatokana na mitambo ya gesi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

"Nazipongeza Taasisi za TPDC na TANESCO kwa kushirikiana na Songas kwani tulikaa pamoja kama wadau ili kuona namna tutakavyotatua tatizo hili, na ndiyo maana angalau megawati 115 zinaendelea kuzalishwa kwa kutumia mitambo ya TPDC." Alisema Samuel

Aidha, alisema kuwa, ukarabati wa mitambo hiyo unafanyika kwa ratiba maalum ili kuweza kutoa uhakika wa mitambo hiyo kuendelea kuzalisha umeme kwa muda mrefu zaidi.

Kwa upande wake, Meneja Mitambo wa Songas, Michael Mngodo alisema kuwa kituo cha umeme cha Songas kina mashine Sita ambapo kwa sasa mashine zinazofanya kazi ni nne na zinazofanyiwa matengenezo ni mashine mbili.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na Bodi na Menejimenti za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kabla ya kukagua kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi.*



*Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa kwanza kushoto), Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka wakiwa katika kikao cha Waziri na Bodi na Menejimenti za TANESCO na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kabla ya kukagua kituo cha umeme cha Songas kilichopo Ubungo mkoani Dar es Salaam*

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, PBPA wajadiliana kuhusu Biashara ya Mafuta nchini

**Na Zuena Msuya, DSM**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, imekutana na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA),kujadili masuala mbalimbali kuhusu sekta ya mafuta nchini.

Kikao hicho kilifanyika jijini Dar es Salaam, Machi 13, 2021, ambapo pamoja na mambo mengine kikao hicho pia kilijadili suala la uagizaji na uingizaji wa mafuta pamoja na uboreshaji wa biashara ya mafuta nchini.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula ambapo aliishauri Wizara pamoja na PBPA kuangalia upya taratibu na sheria zinazosimamia sekta ya Mafuta ili kutoa fursa kubwa kwa Watanzania kushiriki kwa wingi katika biashara ya Mafuta nchini.

Vilevile aliipongeza PBPA kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini muda wote na kwa wakati.



*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Erasto Simon, akitoa maelezo ya namna wakala hiyo inavyofanya kazi kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakati wa kikao cha kujadili biashara ya mafuta nchini, kilichofanyika Jijini Dar es Salaam, Machi 13, 2021.*

Hata hivyo Kitandula alizishauri Mamlaka zenye dhamana ya kusimamia sekta ya mafuta kufanya utafiti wa kina katika mataifa yanayozalisha mafuta ili kuweza kupata bei za chini zaidi kupunguza gharama za uagizaji na kwa watumiaji.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, aliieleza Kamati hiyo kuwa kwa sasa nchi ina mafuta ya kutosheleza mahitaji ya ndani na ziada itakayotumika zaidi ya siku 30.

Hata hivyo Wizara



*Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (aliyesimama) akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakati wa kikao cha kujadili biashara ya Mafuta nchini, kilichofanyika Jijini Dar es Salaam, Machi 13, 2021.*

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, PBPA wajadiliana kuhusu Biashara ya Mafuta nchini

kupitia PBPA inaendelea kujidhatiti katika kudumisha hali ya upatikanaji wa mafuta nchini wakati wote.

Aliweka wazi kuwa, utaratibu uliowekwa na wakala huo, umesaidia kupatikana kwa mafuta nchini wakati wote hata katika kipindi cha mlipuko wa Virusi vya Corona, biashara ya Mafuta nchini haikuathirika.

Vilevile katika kukuza sekta ya Mafuta nchini, Dkt. Kalemani alisema kuwa tayari takribani



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Uongozi wa Wizara ya Nishati Pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ( PBPA) wakisoma nyaraka zinazoeleza biashara ya mafuta nchini, wakati wa kikao kilichofanyika Machi 13, Jijini Dar es Salaam.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (katikati), akizungumza na wajumbe na Uongozi wa Wizara ya Nishati Pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ( PBPA), wakati wa kikao kilichofanyika Machi 13, Jijini Dar es Salaam.*

vijana 100 wa Kike na Kiume wamepata elimu na Mafunzo juu ya Sekta ya mafuta na Gesi katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya Nchi kwa ufadhili wa Serikali.

Asilimia kubwa ya vijana hao wamepata ajira katika taasisi na kampuni za mafuta na Gesi nchini, wengine wakifanya utafiti wa upatikanaji wa mafuta kwenye maeneo tofauti yalioonesha dalili za kuwepo kwa mafuta katika maeneo husika.

# Kampuni Mbili kutekeleza REA III, mzunguko wa Pili, Tabora

**Zuena Msuya, Tabora**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amezitambulisha kampuni mbili zitakazohusika na usambazaji umeme vijijini mkoani Tabora kupitia mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, utakaotekelezwa Kipindi cha miezi 18, kuanzia Sasa.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya( kulia), wakati wa ziara ya kutambulisha wakandarasi watakaotekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alizungumza na wakazi wa kijiji cha Kaselya (hawapo pichani) wilayani Nzega, wakati wa ziara ya kutambulisha wakandarasi watakaotekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021.*

Dkt. Kalemani amezitambulisha kampuni hizo wakati wa ziara ya kukagua baadhi ya vijiji vya mkoa huo ambavyo bado havijafikiwa na Umeme vikiwemo Miyenze na Kanyenye wilayani Uyui, pamoja na Kijiji cha Kaselya wilayani Nzega Mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021.

Katika ziara hiyo Dkt. Kalemani aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, pamoja na viongozi wakuu waandamizi wa Wizara.

Pamoja na mambo mengine, Dkt. Kalemani aliwataka wakandarasi hao kufanya kazi usiku na mchana kwa kasi, ubunifu na usahihi ili kukamilisha mradi huo ndani ya muda uliopangwa ama hata kabla ya muda huo.

Aliwasisitiza wakandarasi hao kutumia vijana walio katika eneo la mradi kufanya kazi zisizohitaji

# Kampuni Mbili kutekeleza REA III, mzunguko wa Pili, Tabora



*Wakazi wa Kijiji cha Kaselya wilayani Nzega, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati wa ziara ya kutambulisha wakandarasi watakaotekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme vijijini Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021.*



*Wakandarasi kutoka Kampuni ya kizalendo ya Sillo iliyopewa dhamana ya kutekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili, wakimsikiliza wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati wa ziara ya kutambulisha wakandarasi watakaotekeleza mradi huo, mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021.*

taaluma maalum kama vile kuchimba mashimo, kuvuta nyaya na nyingine kama hizo ili kunufaika na uwepo wa mradi huo.

Zaidi ya shilingi Bilioni 108.2 zitatumika kutekeleza mradi wa usambazaji wa Umeme katika vijiji 299 vilivyosalia katika mkoa huo wenye jumla ya vijiji 725.

Tayari vijiji 426 vimepata umeme katika wilaya zote za mkoa huo wenye wilaya Saba.

Wilaya hizo ni Tabora Mjini, Kaliua, Uyui, Nzega, Urambo, Sikonge na Igunga.

Kampuni zilizopata dhamana ya kutekeleza mradi huo mkoani humo ni Kampuni ya kizalendo ya Sillo pamoja na Kampuni ya kigeni ya Ceylex kutoka nchini Sri-lanka.

Kwa Upande wake Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, alitilia mkazo maelekezo yaliyotolewa kwa wakandarasi hao na kuwaeleza kuwa, Serikali imewaamini na kuwapa dhamana kubwa kutekeleza mradi huo hivyo wakamilishe kazi hiyo kama mkataba unavyoelekeza.

Wakili Byabato alisema kuwa, wakandarasi hao wakikamilisha kwa wakati mradi huo kwa kumaliza kuunganisha vijiji vyote vilivyosalia, Tanzania itaandika historia mpya kwa bara la Afrika, licha ya kuwa ya kwanza kwa kuunganisha umeme kwenye vijiji vingi kwa nchi za Afrika.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiwatunza Wanafunzi wa shule ya sekondari Kanyeye walioimba shairi, wakati wa ziara ya kutambulisha wakandarasi watakaotekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili mkoani Tabora, iliyofanyika Machi 16, 2021. Wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, yakagua Mradi wa REA, Sengerema

**Na Zuena Msuya, Mwanza**

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imekagua maendeleo ya mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini, pamoja na kuwasha Umeme katika Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Akizungumza katika ziara hiyo iliyofanyika, Machi 17,2021, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Saif Gulamali aliwaeleza wananchi kuwa Serikali imetumia gharama kubwa kuhakikisha miundombinu ya umeme inasambazwa katika vijiji vyote nchini, ili kila mtanzania aweze kumudu gharama nafuu ya kuunganishiwa umeme.

Aidha, Gulamali alitoa wito kwa watanzania wote ambao tayari miundombinu ya umeme imesambazwa katika maeneo yao kuhakikisha wanatumia umeme huo kufanya shughuli za kiuchumi zitakazoweletea maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Tabaruka, wakati wa ziara ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme Vijijini na kuwasha Umeme katika shule ya Sekondari Tamabu, katika Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Machi 17,2021.*




*Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Saif Gulamali (wa tatu kushoto) na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) pamoja na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwasha Umeme katika shule ya Sekondari Tamabu, katika Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Machi 17,2021.*

Akitolea mfano kuanzishwa kwa viwanda vya aina mbalimbali vya kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo, ufugaji pamoja uvuvi kwa kuwa Tanzania nzima imejaliwa kuwa na ardhi yenye rutuba kwa kilimo, kuwa na mifugo ya aina mbalimbali, na maeneo ya uvuvi.

Kwa upande wake Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, aliwataka wananchi wote kuweka umeme katika nyumba zao ili

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, yakagua Mradi wa REA, Sengerema

kuithibitishia Serikali kuwa fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya kuwapatia maendeleo wananchi wake zinatumika ipasavyo kwa kutoa matokeo chanya.

Aliendelea kuwasisitiza wananchi kuendelea kutandaza nyaya katika nyumba zao pamoja na kulipia gharama za kuunganishiwa umeme kwa sababu utawafikia wakati wowote kwa kuwa serikali imedhamiria kupeleka umeme kwa wananchi wote.

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, aliwataka Viongozi wa Serikali za Vijiji, pamoja na Kata, kuhakikisha wanalipia gharama za kuunganisha umeme katika taasisi za umma zikiwemo, vituo vya huduma za afya, shule, pamoja na taasisi za dini kwakuwa umeme ukiwekwa katika maeneo hayo utawanufaisha watu wote kwakuwa watakuwa wakipata huduma maeneo hayo.

Vilevile kutenga na kuonyesha maeneo yatakayojengwa majengo hayo kusaidia wakandarasi kusogeza karibu miundombinu ya umeme,ili iwe rahisi kwa majengo hayo kuunganishiwa umeme pindi ujenzi wake utakapokamilika na kuanza kutumika.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Tabaruka, wakati wa ziara ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini na kuwasha Umeme katika shule ya Sekondari Tamabu, katika Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Machi 17,2021.*



*Wanafunzi wa shule ya sekondari Tamabu wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani( hayupo pichani), wakati wa ziara ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini na kuwasha Umeme katika shule ya Sekondari Tamabu, katika  Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Machi 17,2021.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani( hayupo pichani), wakati wa ziara ya wajumbe hao ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini na kuwasha Umeme katika shule ya Sekondari Tamabu, katika Kijiji cha Tabaruka wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Machi 17,2021.*

# Waziri wa Nishati aweka jiwe la msingi Ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme Simiyu

**Na Zuena Msuya, Simiyu**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameweka jiwe la msingi na kuzindua Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Imalilo kilichopo wilayani Bariadi mkoani Simiyu.

Akizungumza wakati akiweka jiwe la Msingi, Machi 3, 2021, Dkt. Kalemani alisema kuwa Ujenzi wa kituo hicho utakamilika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuanzia sasa.

Aidha alisema kuwaujenzi wa kituo hicho unatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kutumia fedha za ndani shilingi Bilioni 75.



*Waziri wa Nishat, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akiweka jiwe la msingi na kuzindua Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Imalilo kilichopo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Machi 3, 2021.*



*Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Imalilo wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi na kuzindua Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Imalilo kilichopo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Machi 3, 2021.*

Vilevile alisema kuwa Serikali imetoa kiasi cha zaidi ya shilingi Milioni 47, kwa ajili ya kuwalipa fidia Wananchi waliopisha eneo la mradi huo.

Kituo hicho

# Waziri wa Nishati aweka jiwe la msingi Ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme Simiyu



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (pili kulia) akipata maelezo kutoka kwa msimamizi wa ujenzi wa kituo hicho kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa kuweka jiwe la msingi na kuzindua Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Imalilo kilichopo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Machi 3, 2021.*

kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kizalisha takribani Megawati 100, zitakazo tumika ndani ya mkoa huo na mikoa jirani.

"Umeme utakaozalishwa hapa ni mkubwa utauwezesha mkoa huu na mikoa jirani kuendesha shughuli za viwandani, na uwekezaji wa aina yoyote unaohitaji umeme mwingi", alisema Dkt. Kalemani.

Alisema TANESCO wamekuwa wakitekeleza miradi kama hiyo nchi nzima ambapo mpaka sasa tayari wamejenga Vituo vikubwa kama hicho na wanatekeleza miradi mingine kama hiyo 24 kati ya 134 inayotarajiwa kujengwa nchi nzima.

Dkt. Kalemani aliagiza kuwa, kazi zote zisizohitaji taaluma maalum ikiwemo ya vibarua, wapewe vipaumbele watu wanaozunguka eneo hilo na maeneo jirani kwa kuwa ndiyo walinzi wakubwa wa mradi huo.

Hata hivyo alitoa siku mbili kwa TANESCO, kukamilisha kulipa fidia watu Watano ambao bado hawajalipwa fidia kutokana na changamoto ya majina kutofautiana katika vitambulisho, Hundi pamoja na nyaraka za malipo.

Aliwatoa hofu wananchi hao kuwa tayari changamoto hiyo imetatuliwa na muda wote watalipwa fedha zao kwa kuwa zipo tayari.

Kuhusu usambazaji wa Umeme vijijini, aliwaeleza wananchi wa mkoa huo, kujiandaa kwa kutandaza nyaya katika nyumba zao kwa kuwa mradi wa usambazaji wa Umeme Vijijini (REA III) mzunguko wa pili utamaliza usambazaji wa Umeme katika vijiji vyote nchini ambavyo bado havijafikiwa na Umeme.

Aliwasisitiza kuwa bei halisi ya kuunganishiwa Umeme ni shilingi 27,000 tu.

Na zoezi hilo litakamilika ndani ya miezi 24, kusambaza vijiji vyote nchini.

# Mtambo wa umeme Kidatu ufanye kazi ndani ya siku 15 - Dkt. Kalemani

**Na Teresia Mhagama, Morogoro**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhakikisha kuwa, mtambo namba mbili wenye uwezo wa megawati 51 katika kituo cha umeme cha Kidatu, unarekebishwa ndani ya siku 15 ili kituo hicho kizalishe umeme kulingana na uwezo wake ambao ni megawati 204.

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo, tarehe 1 Machi, 2021 mara baada ya kukagua kituo hicho kilichopo mkoani Morogoro, na kukuta mtambo huo haufanyi kazi kutoka mwezi Septemba mwaka 2020.

" Nimetembelea eneo la mgodi na kukuta mashine moja kati ya nne zilizopo haizalishi umeme na nimefuatilia kwa watalaam wamesema bado wapo kwenye mchakato wa kununua spea ili wafunge kwenye mashine husika, kuna shida ya manunuzi hapa, kuna maafisa wamekalia kazi kutoka mwezi Septemba hadi sasa, jambo ambalo limeathiri upatikanaji umeme wa kutosha." Alisema Dkt. Kalemani



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani ( wa Tatu kushoto) pamoja na watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakiwa katika Bwawa la Kidatu mkoani Morogoro. Kulia kwa Waziri ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga na wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt.Tito Mwinuka.*

Kutokana na hilo, Dkt. Kalemani alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, kuwachukulia hatua maofisa wawili wanaohusika na manunuzi, pamoja na Meneja anayesimamia Kituo cha umeme cha Kidatu.

Aidha, akiwa kwenye kituo hicho, Dkt. Kalemani alikagua mitambo ya kupoza umeme na kukuta mashine moja haifanyi kazi kutoka Septemba



*Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (katikati), pamoja na watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakiwa katika chumba cha kuongozea mitambo katika kituo cha umeme cha Kidatu mkoani Morogoro.*

# Mtambo wa umeme Kidatu ufanye kazi ndani ya siku 15 - Dkt. Kalemani

2020 na kuagiza kuwa, ndani ya mwezi mmoja ifungwe mashine mpya ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika na msimamizi wa mitambo hiyo achukuliwe hatua.

Vilevile, Dkt kalemani alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kuhakikisha kuwa matengenezo yoyote ya mitambo ya umeme nchini hayachukui zaidi ya siku Kumi.

Kuhusu vifaa vya kuzuia radi katika njia za usafirishaji umeme, Dkt. Kalemani aliiagiza TANESCO kununua vifaa hivyo ndani ya siku 17 ili hata mvua yenye radi inaponyesha, isiathiri upatikanaji wa umeme.

Akizungumzia hali ya maji katika Bwawa la Kidatu, Dkt. Kalemani alisema kuwa, bwawa hilo lina maji ya kutosha kuzalisha umeme unaotakiwa.

Katika ziara hiyo, Waziri wa Nishati aliambatana na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt.Tito Mwinuka na waatendaji wengine.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mbele, katikati), akikagua kituo cha kupoza umeme katika Kituo cha umeme cha Kidatu mkoani Morogoro. Pamoja naye ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mara baada ya kukagua kituo cha kupoza umeme cha Kidatu mkoani Morogoro. Kushoto kwake ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na kulia kwake ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga.*

# Dkt. Kalemani aagiza ujenzi wa kituo cha umeme Ifakara uanze ndani ya siku Kumi

**Na Teresia Mhagama, Morogoro**

Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Medard Kalemani, amemuagiza mkandarasi, kampuni ya AEE POWER EPC S.A.U kuanza ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme katika Mji wa Ifakara ndani ya siku Kumi, ili kuimarisha hali ya upatikanaji umeme katika Wilaya ya Kilombero pamoja na Ulanga mkoani Morogoro.



*Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (kulia) akizungumza na wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko, Wilayani Ulanga, Mkoa wa Morogoro ambapo ameagiza kuwa migodi ya wachimbaji hao iunganishwe na umeme ndani ya Wiki Moja. Wa Tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngollo Malenya.*

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo tarehe 23 Februari, 2021, wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro baada ya kufika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho na kubaini kuwa, kazi za ujenzi hazijaanza licha ya Mkataba kusainiwa mwezi Aprili mwaka jana.



*Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (katikati), akisisitiza jambo wakati akizungumza na wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko, Wilayani Ulanga, Mkoa wa Morogoro ambapo ameagiza kuwa migodi ya wachimbaji hao iunganishwe na umeme ndani ya Wiki Moja. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Ulanga, Mhe. Salim Almas*

“Haiwezekani mkataba usainiwe kutoka Aprili mwaka jana, lakini hata msingi hamjaweka, hapa kuna uwanja tu, mi nilitaka kuja kuona kazi zinazofanyika, si uwanja, hivyo naagiza Bodi ya Wakala wa Nishati

# Dkt. Kalemani aagiza ujenzi wa kituo cha umeme Ifakara uanze ndani ya siku Kumi



*Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa Tatu kutoka kulia) akikagua kazi ya ujenzi wa kituo kipya cha umeme katika Mji wa Ifakara, wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro. Pamoja naye ni Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, (wa kwanza kushoto), Mbunge wa Kilombero, Mhe. Aboubakar Assenga (wa Pili kulia), pamoja na watendaji kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*

Vijijini , Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wawe wameshafika katika eneo hili ifikapo tarehe 5 Mwezi Machi ili kuhakikisha ujenzi unaanza." Alisema Dkt. Kalemani

Waziri wa Nishati, alisema kuwa, Wilaya ya Kilombero na Ulanga zina changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa sababu zinapata umeme kutoka vituo vya Kihansi na Kidatu ambavyo vipo mbali, na kupelekea Wilaya hizo kupata umeme hafifu.

Aliongeza kuwa, jumla ya shilingi Bilioni 23 zimetolewa na Serikali ya Tanzania pamoja na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho hivyo hakuna sababu ya kuchelewesha ujenzi wa kituo husika, ambacho kinapaswa kukamilika mwezi Aprili mwaka 2022.

Aidha, akiwa katika Mji wa Ifakara, Dkt. Kalemani alitoa agizo kuwa, wananchi wanaoishi katika vitongoji, vijiji na mitaa iliyo pembezoni mwa miji na inafanana na vijiji, waunganishiwe umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu na si zaidi ya hapo.

Awali, Dkt. Kalemani alifanya ziara katika Wilaya ya Ulanga iliyokuwa na lengo la kukagua eneo la wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko ili kuweza kuwapelekea nishati ya umeme itakayowawezesha kufanya uchimbaji wenye tija.

Akiwa wilayani humo. Dkt. Kalemani aliliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji hao wadogo kuanzia wiki ijayo na kwamba kazi hiyo ifanyike kwa takriban kipindi cha mwezi mmoja.

Alisema kuwa gharama ya kupeleka umeme kwenye migodi hiyo ni takribani shilingi milioni 400 ambazo zipo na kwamba wananchi hao wataunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Vilevile, alitoa agizo kwa watendaji wa vijiji kote nchini kuhakikisha kuwa wanatenga fedha kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye Taasisi za Umma kwenye vijiji vyao ili kuwapa wananchi huduma bora ambapo gharama ya kuunganisha umeme kwenye Taasisi hizo ni shilingi 27,000 tu.

# Dkt Kalemani atoa angalizo kwa TANESCO

**Na Teresia Mhagama, Chato**

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani ametoa angalizo kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa, wamebakiwa na mwezi mmoja na nusu tu wa kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia umeme nchini.

Dkt. Kalemani alitoa angalizo hilo tarehe 17 Februari, 2021, wilayani Chato, Mkoa wa Geita wakati alipofanya ziara ya kukagua miundombinu ya umeme pamoja na kuwasha umeme katika Kitongoji cha Mwamatome na Mkombozi wilayani humo.

"Nilitoa muda wa miezi mitatu wa kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia nchi nzima, mwezi mmoja na nusu tayari



*Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika moja ya nyumba zilizounganishiwa umeme kwenye Kitongoji cha Mwamatome, Kata ya Bwongera, wilayani Chato, Mkoa wa Geita.*



*Nyumba ya Ibada katika Kitongoji cha Mkombozi, Kata ya Muganza, wilayani Chato ambayo imeunganishiwa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini.*

# Dkt Kalemani atoa angalizo kwa TANESCO



*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati akizungumza na wananchi wa Kitongoji wa Mwamatome, wilayani Chato, Mkoa wa Geita.*



*Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika Kitongoji cha Mkombozi, Kata ya Muganza, wilayani Chato, Mkoa wa Geita. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho.*

mmeshautumia, sasa mmebakiwa na mwezi mmoja na nusu tu, hivyo waunganishieni umeme wateja wote waliolipia." Alisema Dkt. Kalemani

Kuhusu wateja ambao wanasubiri kupimiwa maeneo yao ili kuunganishwa umeme, amesema kuwa, alishatoa agizo kwa wapimaji wa maeneo wa TANESCO, (surveyors) kununuliwa pikipiki ili kukamilisha upimaji wa maeneo na kwamba ifikapo mwisho wa mwezi wa Pili wawe wameshanunuliwa pikipiki hizo.

Akizungumza na wananchi wa vitongoji hivyo, Dkt.Medard Kalemani amesisitiza kuhusu matumizi ya kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) ambacho kinawawezesha wananchi kupata umeme bila kuingia gharama za kufunga mfumo wa nyaya katika nyumba.

Pia, alisisitiza kuwa, bei ya kuunganisha umeme vijijini ni shilingi 27,000 tu na kwamba kila nyumba inastahili kupata umeme.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho, alisema kuwa, kuunganishwa kwa umeme kwenye vitongoji vya Mwamatome na Mkombozi, wilayani humo kutawawezesha wananchi kuweza kufanya biashara mbalimbali na kuanzisha viwanda vidogovidogo.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI







*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*

**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**

Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018

**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*

*Wizara ya Nishati*

*@Nishati2017*

*wizara_ya_nishati_tanzania*

*Wizara ya Nishati*